



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KATIBA NA SHERIA
WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI
(RITA)**



SHERIA YA USAJILI WA WADHAMINI SURA YA 318 TOLEO LA 2002

**KUONGEZA MUDA WA KUFANYA MAREJEO YA KATIBA ZA TAASISI/
ASASI AMBAZO ZIMESAJILIWA KATIKA OFISI YA KABIDHI WASII
MKUU/RITA.**

REJEA NOTISI ILIYOTOLEWA TAREHE 25 JULAI 2022 ILIYOWATAKA WADHAMINI WA TAASISI/ASASI ZOTE ZILIZOSAJILIWA NA OFISI YA KABIDHI WASII MKUU/RITA KUFANYA MAREJEO YA KATIBA ZA TAASISI ZAO KWA KUFANYA MAREKEBISHO ILI KUZIBORESHA.

NAPENDA KUWAJULISHA WADHAMINI WOTE WA TAASISI/ASASI HUSIKA KWAMBA NIMEONGEZA MUDA WA MIEZI MITATU ILI KUTOA NAFASI KWA TAASISI ZOTE KUWEZA KUKAMILISHA MAREKEBISHO HAYO. HIVYO ZOEZI HILI LITAKAMILIKA TAREHE 7 FEBRUARI 2023.

PIA NAZIKUMBUSHA BODI ZOTE ZA WADHAMINI ZILIZOSAJILIWA NA OFISI YA KABIDHI WASII MKUU/RITA KULETA MAREJESHO YAO YA MWAKA KWA KUJAZA FOMU T.1.5 NA KUWEKA MAWASILIANO IKIWA NI PAMOJA NA NAMBA ZA SIMU NA BARUA PEPE ZINAZOFANYA KAZI.

NATOA RAI KWA WADHAMINI WOTE KUZINGATIA MUDA ULIOTOLEWA. AIDHA, WADHAMINI WANAELEKEZWA KUZINGATIA MUONGOZO WA KUFANYA MABADILIKO YA KATIBA, KATIBA YA MFANO NA MAELEZO MENGINE YAMO KATIKA TOVUTI YA WAKALA (www.rita.go.tz)

Kwa maelezo zaidi piga simu bila malipo kwa namba 0800117482

**ANGELA K. ANATORY
KABIDHI WASII MKUU NA AFISA MTENDAJI MKUU**